PO BOX 11699
TACOMA WA 98411-669

Miadi ya Mahojiano ya Mwombaji
Interview Appointment for Applicant

Washington State Department of Social & Health Services
Transforming lives

Date

Client's Name and Address

Nambari ya TTY / TDD: 800-209-5446
Nambari ya Simu ya Bure: 877-501-2233

Namba ya ID ya Mteja: Client ID

Mpendwa Client's Name :

Tumepokea maombi yako mnamo Date . Unapaswa kukamilisha mahojiano hadi mnamo Date . Unaweza kutupigia kwa nambari 877-501-2233 au kwa kuja ofisini. Masaa yetu ya mahojiano ni Jumatatu hadi Ijumaa 8:00 a.m. na 3:00 p.m. ispokua katika sikukuu za jimbo.

Sehemu:
CSO Name and Street Address

Ikiwa hatutasikia kutoka kwako hadi mnamo Date , ombi lako la ☐ Chakula cha Msingi (Basic Food) ☐ Fedha taslimu (Cash) litakataliwa.

Ombi lako la msaada litakataliwa bila ya kufanyiwa mahojiano.

Hii hapa ni orodha ya vitu ambavyo unaweza ukahitajia kwa ajili ya mahojiano yako:

- Nambari za Usalama wa Jamii kwa ajili ya watu ambao unawafanyia maombi
- Uthibitisho wa urai au hali ya kisheria ya kigeni kama vile pasipoti ya Kimarekani, rekodi za kuzaliwa, nyaraka za uhamiaji.
- Uthibitisho wa utambulisho kama vile ID yenye picha
- Uthibitisho wa kipato kama vile nakala za cheki, risiti za cheki, barua au taarifa kutoka kwa mtu yoyote aliyeipa kaya yako pesa.
- Uthibitisho wa vyanzo ambavyo huenda unavyo kama vile usajili wa gari, taarifa za benki, akiba, bondi, sera za bima ya maisha
- Uthibitisho wa gharama za huduma ya matunzo ya mtoto au huduma ya matunzo ya mtu mzima tegemezi kama vile risiti kutoka kwa mtoa huduma
- Uthibitisho wa gharama za makazi kama vile malipo ya rehani ya jengo, malipo ya kodi ya eneo, bima ya mmiliki wa nyumba, risiti za upangishaji, nakala ya ukodishaji, bili za umeme, maji, gesi nk. barua kutoka kwa mwenyenyumba wako
- Uthibitisho mwingine kama vile bili za matibabu ambazo hazijalipwa, malipo ya bima ya afya, mabadiliko ya uhamiaji wako au hali ya uraia, mimba na tarehe ya kujifungua, usaidizi wa kuasili au malipo ya matunzo ya malezi

Unaweza:

- Kufanya maombi ya ruzuku, kutuma uhakiki, au kuripoti mabadiliko katika www.washingtonconnection.org
- Tutumie taarifa kwa faksi kwa nambari 888-338-7410

Andika ID yako ya mteja katika nakala zote unazotutumia. ID yako ya mteja ni .

Kwa kuwasiliana na meneja wa kesi wa WorkFirst au mfanyakazi wa kijamii, piga Phone Number (include are

Piga 877-501-2233 ili kufanya maombi au uhakiki, kuripoti mabadiliko, au kuuliza maswali.

Tafadhali piga simu ikiwa una maswali kuhusu barua hii.

Viambatanisho: DSHS 14-113 Haki za Mteja na Majukumu

Haki zako za Msaada wa Fedha taslimu na Chakula na Majukumu

Your Cash and Food Assistance Rights and Responsibilities

JINA LA MTEJA (MKUU WA KAYA)
NAMBARI YA UTAMBULISHO WA MTEJA:

Majukumu Yako (Unapaswa)

- **Kutupa taarifa tunayohitaji ili kuamua kama unastahiki.**
- **Kutupa uthibitisho pale unapohitajika.** Tunaweza kukupatia. Taarifa unayoipatia idara inategemea uthibitisho wa watumishi wa muungano na wa taifa. Uthibitisho unaweza kukusanya mawasiliano ya ufuatiliaji kutoka kwa watumishi wa idara wakiwemo wachunguzi wa udanganyifu.
- **Taarifa iliyoripotiwa kwa Idara ya Huduma za Kijamii na Afya** inaweza kuathiri ustahiki wa bima ya huduma ya afya inayosimamiwa na Mamlaka ya Huduma ya Afya na Soko la Ruzuku ya Afya.
- **Ripoti mabadiliko** (kwa mfano, anwani, kipato, n.k.) kama inavyotakiwa katika WAC 388-418-0005. Ziripoti ifikapo tarehe 10 ya mwezi ujao.
- **Shirikiana na Kitengo cha Msaada wa Mtoto (DCS)** kama unakubali msaada wa TANF. Unatakiwa kuisaidia DCS kuanzisha, kurekebisha, au kutia nguvu msaada wa mtoto ambaye yuko kwenye uangalizi wako, na kuanzisha ubaba (kama ni muhimu). Unaweza kukataa kushirikiana na DCS kama utaweza kuonyesha kuwa una sababu nzuri ya kuamini kwamba kushirikiana na DCS kutakuweka wewe, watoto wako, au watoto ambao wako kwenye uangalizi wako kwenye hatari ya madhara kutoka kwa mzazi asiyekuwa msimamizi.
- **Omba** na fanya jihudi za kutosha ili kupata pato linalowezekana kutoka kwenye vyanzo vingine unapoomba au kupokea msaada wa fedha taslimu.
- **Kamilisha ripoti zanazohitajika na mihutasari.**
- **Fuata mahitaji ya kazi** ya msaada wa fedha taslimu na msaada wa chakula.
- **Tuambie** kama unataka mtu mwengine atumie msaada wako wa chakula kwa niaba yako
- **Shirikiana na mihutasari yetu ya Kudhibiti Ubora.**
- **Tumia msaada wa chakula** kwa kununua chakula cha wanakaya wako tu.
- **Tumia msaada wa fedha taslimu** kwa faida ya wanakaya wako tu.
- **Unatakiwa kutoa namba za Usalama wa Jamii** (SSN) au hali ya uhamiaji kwa watu wanaoomba msaada tu. Kama utachagua kutotoa SSN au hali ya uhamiaji ya wanakaya wasioomba, pato la wanakaya wote na vyanzo bado vitatakiwa kuthibitishwa, kama itahitajika, ili kuamua kufaa.

Haki Zako (Hatuna Budi)

- **Kupokea maombi** yenye jina lako, anwani, na saini au saini ya mwakilishi aliyeidhinishwa.
- **Kukusaidia kujaza fomu za DSHS.**
- **Kufanyia kazi** ombi lako la msaada wa chakula ndani ya silu 7 kama utakuwa na sifa ya huduma ya haraka.
- **Kukupa risiti** kama utaiomba wakati utakapotoa nyaraka.
- Kukupa maamuzi ya maandishi, kwenye kesi nyingi, ndani ya siku 30.
- **Unaweza kukataa kuongea na** mchunguzi wa **Upelelezi wa Mapema wa Udanganyifu** (FRED) kutoka Ofisi ya Udanyanyifu na Maelezo. Hutakiwi kumruhusu mchunguzi aingie ndani ya nyumba yako. Unaweza kumwomba mchunguzi aje wakati mwingine. Hili halitaathiri kufaa kwako kwa msaada.
- **Unaweza kuomba baraza la kiidara** kama hukubaliani na maamuzi yanayofanywa na idara kwenye kesi yangu. Pia unaweza kumwomba msimamizi au mtawala apitie maamuzi au tendo lenye mgogoro bila kuathiri haki zako za baraza la kiidara.
- **Tunatakiwa kukutaarifu** kuhusu kanuni ya miezi 60 ya kikomo cha muda chini ya programu ya Msaada wa Muda wa Familia Maskini. Kikomo hichi cha muda hakitumiki kwenye Chakula chako cha Msingi, au ruzuku za uangalizi wa mtoto.

Mambo Unayotakiwa Kuyajua Kuhusu Kadi Yako ya EBT

- **Matumizi Mabaya ya Ruzuku:** Ruzuku za chakula na fedha taslimu zinazosambazwa kupitia kadi ya EBT zitaipa DSHS historia ya kumbukumbu kuhusu ulipotumia ruzuku zako. Idara itatumia taarifa ya kumbukumbu kwenye uchunguzi wa matumizi mabaya ya ruzuku za msaada wa fedha taslimu au kubadilishana kwa ruzuku za msaada wa chakula kwa fedha au vitu vingine vya thamani (biashara haramu).
- **Ubadilishaji wa kadi ya EBT:** Tunaweza kudai malipo ya ubadilishaji wa kadi za EBT Tunza kadi yako ya EBT na namba ya kitambulisho chako (PIN).
- **Akiba Kubwa ya Kadi za EBT:** Kama itatokea hutatumia ruzuku zako kwa miezi au ukalimbikiza akiba kubwa baada ya miezi kadhaa, tunaweza kuwasiliana na wewe ili kutoa muhtasari wa hali yako au mahitaji yako ya ruzuku.

Mambo Unayotakiwa Kuyajua (Chakula cha Msingi)

- **Tutatuma taarifa** kwenda wakala nyingine za muungano kuhusu mtu anayeomba Chakula cha Msingi ili kuangalia kama taarifa ni sahihi. Kama taarifa yoyote sio sahihi, mtu anayeomba hawezi kupata Chakula cha Msingi. Kama mtu atatoa taarifa ambayo anajua sio sahihi, anaweza kushtakiwa kwa kosa hilo. Adhabu za kuvunja kanuni za Chakula cha Msingi kwa makusudi ni tofauti, kuanzia kuvuliwa sifa ya programu, mpaka faini, au uwezekano wa kifungo.
- **Kama utauza, utajaribu kuuza, utabadilishana au utachangia msaada wako wa chakula** kwa kitu chochote cha thamani kama vile fedha taslimu, dawa za kulevya, silaha, au kitu kingine chochote mbali na chakula kutoka kwa muuzaji wa rejareja aliyeidhinishwa (biashara haramu), unaweza kuvuliwa sifa ya kupokea ruzuku za msaada wa chakula kwa kiwango cha chini cha mwaka mmoja mpaka kiwango cha juu cha kuvuliwa sifa maisha yote kwa kosa la kwanza. Uvuliwaji huu wa sifa utaendelea hata kama utaondoka Jimbo la Washington na uombe ruzuku kwenye jimbo lingine.
- **Kama utahitajika kushiriki kwenye mahitaji ya kazi ya Chakula cha Msingi,** na ushindwe kushiriki, unaweza kuvuliwa sifa kwa mwezi mmoja na mpaka utekeleze mahitaji ya kwanza yaliyokushinda; miezi mitatu na mpaka utekeleze mahitaji ya pili yaliyokushinda; na miezi sita na mpaka utekeleze mahitaji ya tatu na kila mara ni hivyo.
- **Unaweza kuondolewa kwenye mpango wa Chakula cha Msingi** kwa kuvunja kanuni za mpango wa Chakula cha Msingi kama ilivyoelezwa kwenye onyo ya adhabu ya Chakula cha Msingi iliyoorodheshwa kwenye ukurasa huu.
- **Ripoti matumizi ya kaya kama unataka idara iingize gharama hizi kwa ajili ya Chakula cha Msingi.** Kama hutaripoti na kutoa ushahidi wa matumizi haya, hivyo unatamka kwamba hutaki tutumie matumizi haya ili kuamua kama unaweza kupata Chakula cha Msingi cha ziada.

Mambo Unayotakiwa Kuyajua (Fedha Taslimu)

- **Kwa kupata Msaada wa Muda wa Familia Maskini (TANF)** unakabidhi haki za msaada wa mtoto na mke/mume wako kwenye Kitengo cha Msaada wa Mtoto. Hii inamaanisha kwamba DCS inaweza kuhifadhi msaada wako, mpaka kufikia kiasi cha msaada wa umma ulichokipokea. **Unatakiwa kuieleza DCS haraka kama ulipokea malipo ya msaada wa mtoto au ruzuku** kwa ajili ya mtoto ulipokuwa TANF.
- **Kama utasimama kupokea TANF** unatakiwa kuieleza DCS kuhusu mabadiliko yoyote ambayo yanaathiri msaada wa mtoto, kama vile mtoto amehama au anwani yangu imebadilika.
- **Kama utapata TANF, unaweza kuomba fedha ya ziada** ya kusaidia kulipa gharama za makazi ya muda ya dharura.

Kwa mujibu wa sheria ya Muungano ya haki za raia na sera na kanuni za haki za raia za Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), USDA, Mawakala wake, ofisi, na waajiriwa, na vyama vinavyoshiriki au kusimamia mipango ya USDA wanapigwa marufuku kufanya ubaguzi wa kijamii, rangi, asili ya utaifa, dini, jinsia, utambuzi wa jinsia (ikiwemo maneno ya jinsia), mwelekeo wa kijinsia, ulemavu, umri, hali ya ndoa, hali ya familia / wazazi, pato linalotoka katika mpango wa msaada wa umma, itikadi za kisiasa, au ulipizaji kisasi au uhusiano wa shughuli ya hapo kabla ya haki za raia, katika mpango au shughuli yoyote iliyofanywa au iliyoanzishwa na USDA (si misingi yote inaendana na mipango yote). Mida ya mwisho ya kuandikisha dawa na malalamiko inatofautiana kutokana na mpango.

Watu wenye ulemavu ambao wanahitaji nyenzo mbadala za mawasiliano kwa ajili ya taarifa ya mpango (mfano: Breli, maandishi makubwa, tepu ya kusikia, Lugha yenye Alama za Kimarekani, n.k.) wanatakiwa kuwasiliana na wakala husika au USDA's TARGET Center kwa (202) 720-2600 (voice and TTY) au wasiliana na USDA kupitia the Federal Relay Service kwa (800) 877-8339. Kwa kuongezea, taarifa ya mpango inaweza kupatikana kwa lugha nyingine isiyokuwa Kiingereza.

Kuandikisha malalamiko ya ubaguzi wa mpango, kamilisha Fomu ya Malalamiko ya Ubaguzi ya mpango wa USDA, AD-3027, inapatikana mtandaoni katika http://www.ascr.usda.gov/complaint_filing_cust.html na katika ofisi yoyote ya USDA au andika barua yenye anwani ya USDA na ndani ya barua weka taarifa yote iliyoombwa kwenye fomu. Kuomba nakala ya fomu ya malalamiko, piga simu (866) 632-9992. Tuma fomu yako kamili au barua kwenda USDA kwa:

1. Barua: U.S. Department of Agriculture
   Office of the Assistant Secretary for Civil Rights
   1400 Independence Ave, SW
   Washington, D.C. 20250-9410;
2. Faksi: (202) 690-7442; au
3. Baruapepe: program.intake@usda.gov

USDA ni mtoaji wa nafasi sawa, mwajiri, na mtoaji wa mikopo.

Kwa kutia saini hapo chini, ninatamka kwamba nimepata haki zangu na majukumumu ya kupokea ruzuku za DSHS na programu nilizoelezewa. Ninatambua kama nitakataa kusaini nyaraka hii haitaathiri kufaa kwangu ila bado nashikiliwa kama mhusika wa mahitaji ya programu na nitahusika na adhabu stahiki za programu au za makosa.

SAINI YA MWOMBAJI	TAREHE	SAINI YA MWENZI WA MWOMBAJI	TAREHE

ACES ID YA MTUMISHI WA DSHS: ☐ Amekataa kusaini.